



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Mei 19, 2022

TAARIFA KWA UMMA

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA AKABIDHIWATUZO YA PONGEZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratus leo Mei 19, 2022 amekabidhiwa Tuzo ya pongezi kutoka kwa Shirika la Milo Sayuni Orphanage (MISO).

Wakati wa makabidhiano hayo Meneja wa Mradi Bw. William Ngailo amesema kuwa, ***Tuzo hii ya pongezi tunakukabidhi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na tunakushukuru kwa ushirikiano wako kwa kipindi chote, tangu mwaka 2016 hadi mwaka 2021 mradi huu umeweza kufanikiwa na kuzifikia kata 16 za Wilaya ya Ludewa, Shirika la Milo Sayuni Orphanage (MISO) lipo Wilaya ya Ludewa na linafanya kazi mbalimbali haswa katika sekta ya Afya, Elimu na Uchumi.***

Aidha Shirika la Milo Sayuni Orphanage limefanikiwa kuwafikia watoto wote wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa kutoa msaada wa mahitaji mbalimbali kama vile vifaa vyote vya shule, kuwakatia bima za afya na pia tumewafikia watoto wote wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa kutekeleza mradi ulio itwa kwa jina la Mradi wa USAID Kizazi kipya.

CHRISPIN B. KALINGA
AFISA HABARI (W),
LUDEWA